



Siku niliyo ondoka nyumbani kuelekea jijini

- ✍ Lesley Koyi, Ursula Nafula
- 👤 Brian Wambi
- 💬 Ursula Nafula
- 💬 Kiswahili
- 📊 Level 3



Kituo kidogo cha mabasi kijijini mwetu kilijaa shughuli za watu na mabasi. Basi nyingi zilikuwa zimejaza mizigo. Chini, palikuwa na mizigo zaidi ya kupakia. Kondakta waliita majina tofauti ya mahali basi zilielekea.



“Kwenda jijini! Kwenda jijini! Kwenda magharibi!” Nilisikia kondakta akiita kwa sauti. Ile ndiyo basi niliyohitaji kupanda kwa usafiri wangu.




Basi la kwenda jijini lilikuwa karibu kujaa, lakini watu zaidi walijishughulisha kutaka kupanda. Baadhi yao walipakia mizigo chini ya basi. Wengine waliweka katika sehemu ya juu.



Abiria wapya walishika tiketi zao huku wakitafuta mahali pa kukaa. Wanawake waliokuwa na watoto wodogo waliwatayarisha kwa safari hiyo ndefu.



Nilipenyeza ndani nikakaa karibu na dirisha. Mtu aliyeketi karibu nami alishika mfuko wa plastiki wa kijani kibichi. Alivaa viatu vilivyozeeka, koti kukuu na alionekana kuwa na wasiwasi.



Niliangalia nje na kutambua kwamba nilikuwa naondoka kijijini mwangu, mahali ambapo nililelewa. Nilikuwa naenda katika jiji kubwa.



Upakiaji mizigo ulikamilika na abiria wakawa wameketi. Wachuuzi walizidi kusukumana kutaka kuingia ndani ya basi ili wauze bidhaa zao. Kila mmoja alitaja kwa sauti majina ya bidhaa alivyokuwa anauza. Maneno yao yalinifurahisha.



Baadhi ya abiria walinunua vinywaji. Wengine wakanunua vitafunwa vidogo na kuanza kutafuna. Wasiokuwa na fedha, kama mimi, walitazama tu.



Shughuli hizi zilikatizwa kwa mlio wa honi ya basi, ishara kwamba tulikuwa tayari kuondoka. Kondakta aliwataka wachuuzi kuondoka ndani ya basi.



Wachuuzi walisukumana huku wakitafuta njia ya kushuka. Wengine wao waliwarudisha abiria chenji zao. Wengine walifanya juhudi za mwisho kuuza bidhaa zao.



Basi lilipoondoka kituoni, nilichungulia dirishani. Nilijiuliza endapo ningerudi na kwenda kijijini kwangu tena.



Safari ilipoendelea, joto lilikuwa jingi ndani ya basi. Niliyafumba macho yangu nikiuia kulala.



Lakini mawazo yangu yalirejea nyumbani. Je, mamangu atakuwa salama? Je, sungura wangu wataleta hela zozote? Je, ndugu yangu atakumbuka kunyunyizia maji miche ya miti yangu?



Njiani, nilikariri jina la mahali mjomba wangu alipoishi katika jiji kubwa. Nilikuwa bado nafikiria wakati nilipopatwa na usingizi.



Baada ya saa tisa, niliamshwa kwa kelele za kuita abiria waliokwenda katika kijiji changu. Nilichukuwa mfuko wangu mdogo na kuruka nje ya basi.



Basi la kurudi lilikuwa linajaa upesi. Muda mfupi baadaye, lingeanza safari ya kwenda mashariki. Jambo la maana kwangu wakati huo lilikuwa kuanza kutafuta nyumba ya mjomba wangu.



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Siku niliyo ondoka nyumbani kuelekea jijini

Written by: Lesley Koyi, Ursula Nafula

Illustrated by: Brian Wambi

Translated by: Ursula Nafula

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).